TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Desemba 12, 2015

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## Tume yalaani hatua za Viongozi kuwaweka rumande watumishi wa umma kwa makosa ya kinidhamu

Hivi karibuni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepokea taarifa kupitia vyombo vya habari za kueleza kuwa baadhi ya Viongozi wa Serikali hususan Wakuu wa Wilaya na Mikoa wamekuwa wakiamuru watumishi wa umma wakamatwe na kuwekwa mahabusu kwa kutowajibika ipasavyo katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiutendaji.

Miongoni mwa matukio ya hivi karibuni ni lile lililojitokeza Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa Mwezi Novemba, 2015 ambapo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni aliwaweka ndani kwa takriban saa sita maofisa ardhi waliochelewa kufika eneo la mkutano kusikiliza mgogoro wa ardhi.

Tukio jingine ni lile lililotokea wiki hii huko Mkoani Mara ambapo Mkuu wa Wilaya ya Musoma aliamuru Afisa Afya kuwekwa rumande kwa kosa la kushindwa kusimamia agizo la kusafisha maeneo yake.

Kwa tathmini ya Tume watumishi hawa walitenda makosa ya kutotii mamlaka za viongozi wao, ambayo ni makosa ya kiutawala. Hivyo hatua za kinidhamu na kiutawala ndizo zilizopaswa kuchukuliwa dhidi yao, na siyo hatua za kuagiza au kutumia polisi kuwakamata watumishi hao kama vile walitenda makosa ya jinai.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inasisitiza kwamba vitendo vya kuwaweka ndani watumishi hao wa umma kwa makosa ya kiutawala

vinavunja haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwani walistahili kuwajibishwa kwa utovu wa nidhamu siyo kuwekwa rumande.

Pamoja na nia nzuri ya kutaka kutatua kero za wananchi na kuhakikisha wanapata haki zao haraka, haiondowi wajibu wa viongozi kuzingatia misingi ya utawala bora na kuheshimu haki za binadamu kama zilivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu zinazotaka kila mtu kuheshimiwa utu wake.

Tume haiungi mkono vitendo vya uzembe, ubadhirifu, rushwa, ufisadi na vya kutotii mamlaka husika vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wa umma. Vivyo hivyo haiungi mkono viongozi kuwaweka ndani watumishi wa umma kwa makosa ya kiutawala, ambayo hayahusiani na tuhuma za jinai.

Mwisho, Tume inashauri kuwa masuala ya kazi yaendeshwe kwa sheria na kanuni za kazi, na kuwa viongozi wazingatie utawala wa sheria.

Imetolewa na:

Bahame Tom Nyanduga
**Mwenyekiti**

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Desemba 12, 2015